



**UTUME WA KWAYA KATOLIKI TANZANIA**  
**TANZANIA EPISCOPAL CONFERENCE**



P.O.BOX 2133, Dar-es-Salaam Tanzania, Tel: +255 222 928 341, Email: [ukwakatatec@gmail.com](mailto:ukwakatatec@gmail.com)

25 Septemba 2024

Kumb: T.UKWAKATA/m1/sep.2024

Wenyeviti wa UKWAKATA  
Majimbo yote Tanzania

**YAH: TUNAPIGA HATUA**

Huku tukimtukuza Mungu na kumshukuru kwa kumaliza salama kongamano la Ekaristi, tunawapongeza wana UKWAKATA kote nchini kwa kuendelea kushiriki vema maadhimisho mbalimbali ya kitaifa yanayofanyikia kwenye majimbo yenu. Katika siku za karibuni, tumekuwa tukishuhudia ufanisi mzuri zaidi kiuimbaji kwenye matukio ya kitaifa kadiri siku zinavyokwenda, ikilinganishwa na huko tulikotoka. Hivyo tunawaalika kupeleka pongezi hizi na ufanuzi wake wote kwa wana-UKWAKATA wote majimboni mwetu.

Mambo mawili makubwa zaidi yaliyoonekana kuchangia ufanisi mkubwa wa uimbaaji kwenye matukio ya kitaifa ya hivi karibuni, na ambayo tungetamani wote tuyajifunze na kuyazingatia kwenye matukio yote ya kitaifa na kimetropolitani ni haya:

**1. UCHAGUZI WA NYIMBO ZINAZOSHIRIKISHA WAAMINI WOTE**

Kwa kiasi kikubwa sana (ingawa si chote) ratiba za nyimbo kwenye matukio haya zilitawaliwa na nyimbo ambazo waamini wote bila kujali wametokea wapi na wapi wanaweza kushiriki kuziimba wakati wa adhimisho. Huko nyuma kulikuwa na mwenendo usio sahihi wa walimu wanaosimamia maandalizi ya tukio kulazimisha kuchomeka nyimbo mpya walizotunga wao au wanazopenda wao kwenye maadhimisho ya kitaifa au kikanda hata mahali ambapo hapana ulazima wa wimbo mpya. Mwenendo huu sasa unaendelea kupungua sana na hivyo kosa hilo limebaki linajitokeza mara mojamoja tu, jambo linaloleta matumaini kwamba huenda litafutika kabisa siku si nydingi.

Sio sahihi na sio ukomavu kutumia wimbo mpya kabisa au ambao haufahamiwi na waamini wengi kwenye tukio la kitaifa au kikanda, kwani pale ni mahali pa kutuunganisha wote na sio kuwafanya baadhi waanze kuwashangaa wenzao wakishiriki sala kwa njia ya wimbo. Hivyo, tunajifunza kwamba wimbo mpya au usiofahamika vyta kutosha kwenye matukio ya uzito huu utumike pale tu ambapo ni lazima sana. Kwa

mfano, ikiwa antifona husika haina wimbo unaofahamika, au souvenir ya mteule, au wimbo ulioandaliwa mahsus kwa ajili ya tukio hilo, au wimbo mwininge wenye sababu njema za lazima kama hizo, huo unaweza kuimbwa mpya ikibidi. Lakini kuimba wimbo mpya sehemu ya wimbo wa kawaida wa matoleo au wa komunyo au Bwana utuhurumie, ni kutoendana na hadhi ya tukio la kitaifa au kikanda ambalo linapaswa kuwaunganisha waamini wote kiraifa au kikanda kutoka maeneo mbalimbali walikotoka.

## 2. MAANDALIZI YA KUTOSHA KWA WOTE WANAOHUSIKA KWENYE KWAYA INAYOIMBA SIKU YA TUKIO

Kama vitengo vyote vya kwaya (waimbaji, walimu, waimbishi/wapimishi/watiribu, wapiga kinanda, wapigaji wa ala nyininge, mwimbaji wa zaburi, nk) wamefanya maandalizi ya kutosha pamoja, mshikamano na uzuri wa uimbaji wao kwenye tukio hauwezi kujificha. Ndiyo maana tunawapongeza UKWAKATA katika majimbo yaliyoandaa matukio ya kitaifa yaliyoongozana hivi karibuni kwa maandalizi mazuri.

Hapa tunajifunza kwamba kufanya maandalizi mazuri pekee hakuna maana yoyote kama dakika za mwisho au siku ya tukio tutaruhusu watu ambaao hawakushiriki maandalizi ya pamoja waje kujichomeka katikati ya waliojiandaa na kulazimisha kuimba, au kuimbisha/kutiribu, au kupiga kinanda, ngoma nk. Ni vema basi wale ambaao kwa sababu zozote hawapati nafasi kushiriki vema maandalizi pamoja na wenzao, licha umuhimu wao mkubwa katika utume wa uimbaji au katika kanisa kwa ujumla, walitende haki adhimisho hasa la kiwango kikubwa kama la kitaifa au kikanda kwa kuwa wavumilivu na kuwaachia waliojiandaa ndio wafanye majukumu kadiri ya maandalizi. Hii itatupa nafasi ya kulipatia kanisa heshima linayostahili. Isitoshe, hii ndiyo desturi njema kwa mwanakwaya hata katika maisha ya siku hadi siku ya kwaya zetu maparokiani.

Pamoja nanyi katika utume,



**BERNARD MWOMBEKI MUKASA**  
Mratibu – UKWAKATA (T)

Nakala:

1. M/kiti – Kamati ya Muziki Mtakatifu (T)

